



NDAKI YA MISITU WANYAMAPORI NA UTALII

GREVILLIA "Silky oak" (*Grevillea robusta*)

Family: Proteaceae



Kimetolewa na
Ndaki ya Misitu Wanyamapori na Utalii,
Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo,
S. L. P 3009,
Chuo Kikuu,
MOROGORO TANZANIA

Tel. Gen. Line 255 023 2603511/4 Ext. 4601
E-mail: forestry@suanet.ac.tz



MAELEZO YA JUMLA

Grevillia inawezekana kuwa inakuzwa zaidi Afrika kuliko katika mashamba ya Australia. Mti uliokuwa vema unaweza kufika urefu wa kati ya mita 20 hadi 30.

Hustawi vema hata katika maeneo zaidi ya mwinuko wa mita 900 na wastani wa hali ya joto la nyuzi 10 hadi 26 Sentigredi

Grevillia inastawi vizuri kote Afrika Mashariki katika maeneo yenye mvua za wastani na mvua nyingi. Katika maeneo mengine inapandwa kwa wingi hata kushindana na mazao ya chakula

Grevillia ina uwezo wa kustahimili aina mbalimbali za udongo uliochanguka, kutoka udongo ulio na tindikali kidogo hadi kiwango cha juu. (Histosols, Inceptisols, and Ultisols).

Pamoja na kwamba Grevillia inakuwa vema katika vitalu na kuoteshwaa mashambani, huwa inamea vema kando kando ya mashamba ya miti, katika maeneo ya wazi ndani ya mashamba.


UKUZAJI KATIKA BUSTANI

Mbegu za Grevillia huoteshwaa katika viriba ili kupata miche mizuri. Pia wakati mwagine maotea yaliyofikisha umri wa wiki 4 hadi 6 huweza kuchukuliwa kwa utaratibu na kuoteshwaa katika viriba ili ifikie ukubwa mzuri na unaofaa kupelekwa shambani. Kwa wastani miche ikifikia urefu wa sentimita 30 inafaa kupelekwa kwa kuoteshwaa shambani.



UKUZAJI

Katika sehemu nyingi hupandwa katika nafasi mita 2.5×2.5 mpaka 3×3 , na ina uwezo wa kuvumilia hali mbali mbali za hewa.



Grevillia inaweza kuvunwa ikiwa na umri kati ya 15 hadi 20

MATUMIZI

▀ Mbao kwa ajili ya matumizi mbalimbali



▀ Chanzo kizuri cha chavua kwa ajili ya nyuki kutengeneza asali



▀ Kivuli katika mashamba ya kahawa na chai



▀ Venia, fanicha na vyombo vya muziki.

